MKATABA WA UPANGISHAJI

MKATABA HUU UMESAINIWA leo tarehe...28........mwezi ...07... mwaka 2023

kati ya

MEKRIDE PAULO MDENYE wa S.L.P 316 NJOMBE (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mpangishaji") kwa upande mmoja,

Na

*RUIYA COMPANY LIMITED* wa NJOMBE (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mpangaji") kwa upande mwingine.

**KWA KUWA MPANGISHAJI** ni **Mmiliki** halali wa shamba lenye ukubwa wa ekari mbili na nusu lililopo katika eneo la **Lupanga**, kijiji cha **Nundu** kata ya **Yakobi** katika wilaya ya Njombe lenye majirani pande zote nne kama barabara kuu Njombe –Ludewa,msitu wa asili,kanuti na mekride Mdenye.

NA ambapo MPANGAJI anapanga eneo hilo kwa ajili ya shughuli za kuchakata magogo

NA KWA KUWA kwa mara ya kwanza mpangishaji aliingia makubaliano ya upangishaji na kampuni ya XIANGFENG WOOD LIMITED ambayo kwa sasa wamewaachia eneo hilo kwa ajili ya kuendelea na uchakataji wa magogo kampuni nyingine iitwayo *RUIYA COMPANY LIMITED :*

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALIANO YAFUATAYO:-

1. KWAMBA, kwa malipo ya kodi ya shilingi laki mbili tu (200,000/=) kwa ekari kwa mwezi na ambapo Mpangaji wa kwanza ameshamlipa jumla ya kiasi cha shilingi milioni sita tu (6,000,000/=) ikiwa ni kodi ya shamba/eneo hilo la ekari mbili na nusu kwa mwaka mzima.

2. KWAMBA,malipo yote yalishalipwa na .kampuni ya XIANGFENG WOOD LIMITED mbele ya ofisi ya mwanasheria ijulikanayo kama MEPHOBOU LAW ATTORNEY iliyopo Njombe.
3. KWAMBA,kwa kuwa kampuni hiyo imehama hivyo mara baada ya mwaka wa mkataba huu kuisha , malipo yote ya upangaji wa eneo hilo yatakuwa yanalipwa na kampuni ya RUIYA COMPANY LIMITED ambao ndio wapangaji wapya kwa sasa.

4. **KWAMBA,** mkataba huu utakuwa ni wa muda wa miaka mitano (5) na unaweza kurudiwa /kuhuishwa tena kwa makubaliano ya pande zote mbili.

5. **KWAMBA,** mkataba huu utaanza rasmi kutumika kuanzia tarehe **12** mwezi **05** mwaka **2023** mpaka tarehe **12** mwezi **05** mwaka **2024**

6. **KWAMBA,** kama mpangaji katimiza masharti yote ya mkataba huu ikiwa ni pamoja na kulipa kodi zote kwa wakati ,mpangishaji au mwakilishi wake hatambughudhi mpangaji katika kipindi chote cha mkataba huu.

7. **KWAMBA,** endapo kutakuwa na mgogoro wowote taratibu za usuluhishi zitakuwa kama ifuatavyo:

   a. Wahusika watakutana kwa pamoja na kumaliza tofauti zao mezani
   b. Kama mgogoro utakuwa haujaisha mgogoro utapelekwa kwa mwenyekiti wa kijiji.
   c. Ikishindikana kwa mwenyekiti wa kijiji mhusika anayedhani hajatendewa haki, ana haki ya kupeleka mgogoro kwenye vyombo vya juu vya sheria.

8. **KUBADILISHWA AU KUBORESHWA KWA MKATABA**
   a. Kwamba ,mpangishaji anayo haki ya kubadili na kuboresha mkataba huu muda wowote kadri hali itakapolazimu ili kukidhi haja ya mabadiliko ya muda na uhitaji wa mpangaji au mpangishaji kwa makubaliano ya pamoja.
   b. Kwamba, endapo mabadiliko hayajamhusisha mpangaji, mkataba ukishaboreshwa utaanza kutumika kipindi cha mkataba unaofuata.
   c. Kwamba,notisi ya mabadiliko ya kodi yatatolewa na mpangishaji si chini ya siku 14 kabla ya mkataba wa zamani kuisha.

9. **KUSITISHWA KWA MKATABA**
   a. Kwamba,notisi ya kusitisha mkataba kwa mpangaji na mpangishaji utafanywa kimaandishi si chini ya siku 14 kabla ya siku ya kukatisha mkataba huo au kabla ya mkataba uliopo kuisha.
   b. Kwamba,Kama usitishwaji utafanywa na mpaangishaji kwa ridhaa yake mwenyewe ,mpangishaji atawajibika kurudisha pesa zote zililzobaki za mkataba, hasara zote kiujumla, pamoja na notisi ya kimaandishi ya siku 14.
   c. Kama, usitishwaji utafanywa mpangaji kwa ridhaa yake mwenyewe, au utafanywa kwa sababu ya mpangaji kukiuka moja ya vipengele katika mkataba huu kodi iliyolipwa haitarudishwa na kama mpangaji anadaiwa kitu chochote atawajibika kulipa kabla ya kuhama vinginevyo taratibu za kisheria za madai zitafuata mkondo wake.

10. **KWAMBA,** sababu zitakazofanya mpangaji asitishiwe mkataba wake ni pale mpangaji atakapochelewesha kodi mara kwa mara bila idhini ya mpangishaji (kodi itahesabika imecheleweshw kama itakuwa ikilipwa zaidi ya siku saba ya tarehe halali ya kulipa kodi hiyo.

11. KWAMBA, chini ya makubaliano haya mpangaji hataruhusiwa kumpangisha mtu mwingine pasipo ridhaa/idhini ya maandishi ya wapangaji/wamiliki wa eneo hilo.
12. KWAMBA, endapo mpangishaji atakuwa amefariki hivyo msimamizi wake wa mirathi ndiye atakayehusika katika kupoke malipo haya kwa manufaa ya warithi wake wote.

13. KWAMBA, mpangaji atawajibika kulipa kodi ya withholding tax kwenye mamlaka/taasisi husika.

14. KWAMBA, ikiwa mpangaji atashindwa kulipa kodi kwa wakati kama ilivyoainishwa katika aya ya 4 ya mkataba huu pasipo kutoa sababu yoyote ya msingi kwa mpangishaji , mpangishaji atakuwa huru/haki ya kuvunja mkataba huu.

15. KWAMBA, ikiwa fungu lolote la mkataba huu litaonekana kuwa batili, basi fungu hilo litabatilishwa, lakini mafungu mengine hayataathiriwa na ubatili wa fungu hilo litakalobatilishwa na pande zote zitaendelea kuwajibika kadiri ya maelezo ya mafungu hayo yatakayobaki kuwa na nguvu kisheria.

16. KWAMBA, mkataba huu ni wa hiari ya pande zote mbili na utatawaliwa na masharti yake, sheria ya Upangaji na sheria nyingine zinazohusika, zitumikazo nchini Tanzania.

PANDE ZOTE MBILI ZIMETIA SAHIHI ZAO KUSHUHUDIA MAKUBALIANO HAYA:

Imetiwa sahihi hapa njombe na huyo
MEKRIDE PAULO MDENYE
leo tarehe .28. mwezi...07... 2023

M.P. Mdenye
SAHIHI YA MPANGISHAJI

Imetiwa sahihi hapa Njombe na huyo
*RUIYA COMPANY LIMITED*
leo tarehe .28. mwezi .07. 2023
JINA:.....Rugiyamu Kamugisha.....
SAHIHI:..................

RUIYA COMPANY LTD * NJOMBE - TANZANIA *

MUHURI

MPANGAJI

MKATABA HUU UMESHUHUDIWA NA:

JINA: HAPPY ILOMO
SAHIHI:..................

WADHIFA: WAKILI

HAPPY ILOMO ADVOCATE, NOTARY PUBLIC & COMMISSIONER FOR OATHS P.O. BOX 508, NJOMBE